Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 6, Issue 1

3rd Safar 1432

7th January, 2011

Yaliyomo

Njia Kumi za 1 - 3

Ahaadeeth Za Najd 3 - 4

NJIA KUMI ZA KUJIKINGA NA MCHAWI, HASIDI NA MWENYE KIJICHO

Mtayarishi: Imaam Ibn al-Qayyim al-Jawziyyah

Walaa Hawla Walaa Quwwata illa Billaah.

Mtu anaweza kujikinga na shari ya hasidi, mchawi na mwenye kijicho kwa njia Kumi zifuatazo:

KUSHIKAMAN NA TAWHEED: Na tunayoyakusudia hapa katika maudhui haya ni Tauheed ar-Ruboobiyyah (kumpwekesha Allaah katika matendo yake). Yaani anatakiwa Muislamu aitakidi yakwamba kila litakalomfika, liwe zuri au baya, basi hilo nin kwa amri na mipango yake Allaah peke yake na wala hakuna mkono wa mtu (kiumbe) yoyote. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Sema halitatusibu (halitupati sisi) ila alilotuandikia Allaah litupate. Yeye ndiye Mola wetu, basi (waislamu) na wamtegemee Allaah tu."** [at-Tawbah:51].

Kwahivyo, mtu anapofikwa na shari, kama vile ya mchawi, hasidi na mwenye kijicho, basi anatakiwa kwanza awe na Imani hii ya ki-tauhidi, au kuwa shari iliyomfika imetokana na Amri na mipango yake Allaah na kwamba hakuna awezae kuiondosha shari hiyo, si mganga wa vitabu wala watunguri wala wa jadi na wala wa kita'alamu ila awezae ni Allaah Peke yake. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى):**"Na kama Allaah akikuangushia madhara (basi) hakuna yeyote awezae kuyaondosha ila Yeye."** [al-An'aam: 17].

Na amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) kumwambia 'Abdillaah Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه):"*Jua yakwamba, Lau Umma wote utakutana ili waweze kukunufaisha kwa jambo fulani hawataweza kukunufaisha ila kwa jambo lile lile ambalo Allaah amekuandikia ulipate. Na pia lau watakutana ili wapange njama za kukudhuru, juu ya jambo (fulani); basi hawataweza kukudhuru ila kwa lile lile jambo ambalo Allaah amekuandikia likufike ...*" Ni hakika kabisa Muislamu atakapokuwa na Imani hii hawezi kuwa na khofu juu ya jambo lolote lile, kutoka kwa mtu yoyote yule. Na wakati huo huo adui yake atamuona si chochote si lolote; bali khofu yake itabakia kwa Allaah Peke yake ambae ndiye anaestahiki kuogopewa kwa kila jambo. Allaah (عز وجلّ) anasema: **"(Nyinyi Waislamu) musiwaogope watu, bali niogopeni Mimi (Allaah)."** [al-Maa'idah:44].

Muislamu anapoelekeza khofu yake kwa Allaah Peke Yake, Allaah hufurahi, na humpa mja wake huyo hifadhi na kinga ya kumlinda na kila shari. Wamesema baadhi ya Salaf: "Anaemuogopa Allaah huogopewa na kila mtu na asiyemuogopa Allaah, haogopewi na yoyote.!"

KUMUABUDU ALLAAH UKWELI WA KUMUABUDU: Kumuabudu Allaah kwa kutekeleza maamrisho yake yote na kujiepusha na makatazo yake yote ni miongoni mwa njia muhimu sana za kujikinga na shari za mchawi, Hasidi na mwenye kijicho. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na kama nyinyi mkisubiri na mkamcha (mkamuabudu) Allaah, hila zao hazitakudhuruni kitu. Hakika Allaah anayajua vizuri yote wanayoyatenda."** [Aal Imraan:120].

Na amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) kumwambia 'Abdillaah Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه): "*Muhifadhi Allaah (kwa kutekeleza maamrisho yake na kujiepusha na makatazo yake) na Yeye atakuhifadhi (kwa kukulinda na shari zote). Muhifadhi Allaah, utamkuta mbele yako siku zote.*"

Kutokana na maelezo ya aya na hadeeth zilizotangulia, imefahamika yakuwa, mchaji Mungu wa kisawasawa hawezi kudhurika na uchawi wala hasadi wala kijicho wala shari ya aina yoyote ile. Hii ni kutokana na kuwa mcha Mungu, mlinzi wake ni Allaah. Sasa ikiwa mtu mlinzi wake ni Allaah ni nani atakaembabaisha? Bila shaka hakuna kiumbe yoyote yule anaeweza kuopambana na nguvu za Allaah, Bwana wa viumbe wote!.

KUFANYA MAMBO KWA IKHLASI: Lazima kwanza tuelewe yakwamba matendo yote ya Muislamu yanamfurahisha Allaah wakati yanapokuwa matendo hayo yanatendwa kwa njia ya ikhlasi (yaani kufanya kwa ajili yake yeye tu). Kwa sababu ikhlasi ndiyo nguzo

ya matendo yote na ni sharti pia ya kufaa kwa matendo hayo. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Wala hawakuamrishwa ila kumuabudu Allaah na kumtakasia dini."** [al-Bayyinah:5]. Baada ya kufahamu hayo yaliyotangulia jua yakwamba ikhlasi pia ni mojawapo ya sababu ambayo inamfanya mtu kupata ulinzi wa Allaah na kuepushwa na mabaya mengi. Allaah anasema kumuhusu Nabii Yusuf (عليه السلام) **"... Tumefanya namna hivi, ili tumuepushie kila jambo la ubaya na la uovu. Hakika yeye alikuwa katika waja wetu waliopewa ikhlasi (waliosafishwa)."** [Yusuf:24]. Amesema Sheikh Abdullaah Saaleh al-Faarisy katika tafsiri ya aya hii: "Ni wajibu kwa mtuy kuitakasa nafsi yake." [Tafsiri ya Sheikh Abdullaah Saaleh al-Faarisy: 3:12]. Tunapata katika aya hii, Nabii ambaye alikuwa ni mwingi wa ikhlasi; Allaah anamuondoshea mabaya na shari na vitimbi vyingi vilivyotokana na watu mbali mbali. Kwahiyo kila Muislamu ambaye atakaefanya mambo yake kwa njia ya ikhlasi basi atapata hifadha ya Allaah kama Nabii Yusuf na Manabii wengine.

KUMTUMAINIA ALLAAH NA KUMTEGEMEA KWA KILA JAMBO: Kumtumainia Allaah ni mojawapo – pia ya zile sababu kuu za kujikinga na jambo asiloliweza mtu katika shari za viumbe wenzake. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na anayemtegemjea Allaah, basi Yeye (Allaah) humtoshea."** [at-Talaaq: 3]. Mtu lau atamtumainia Allaah ukweli wa kumtumainia, hata kama angalizungukwa na viumbe wote wa mbinguni na ardhini ili wamdhuru, angalipata upenyo wa kuwatoka na kupata nusra ya Allaah na wale maadui hao wasingaliweza kumdhuru kwa lolote.

KUFANYA HARAKA KUTUBIA (KUOMBA TOBA NA MSAMAHA KWA ALLAAH): Mtu anapofikwa na jambo lolote lile baya wakati mwengine ni kwa sababu ya madhambi yake (malipo ya matendo yake maovu aliyoyatenda kumfanyia Allaah au binadamu wenzake awe anayajua maovu hayo au hayajui). Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na misiba inayokupateni ni kwa sababu ya yale mliyoyachuma kwa mikono yenu (katika mambo maovu)."** [ash-Shura:30]. Kutokana na madhambi ya mtu, Allaah huzuiya nusra yake wakati maadui wake wanapoelekeza mashambulizi yao dhidi yake. Kwa ajili hiyo basi, ndiyo maana Mtume wetu Muhammad (صلى الله عليه وسلم) alikuwa mara nyingi akiomba Du'ah yake maarufu: *"Ewe Mola wetu wa haki usitusaliti (usiwape nafasi ya kutudhuru na kututesa) – kwa sababu ya madhambi yetu wale ambao hawakuogopi wewe wala hawana huruma na sisi."*

Kwahiyo, bila ya shaka kutubia juu ya maovu yetu ni miongoni mwa sababu kubwa ya kuturudishia sisi ulinzi wa Allaah na nusura yake ambayo itatuokoa wakati wa shari za wachawi, mahasidi na wenye vijicho.

KUTOA SADAKA NA KUWATENDEA IHSANI (WEMA) WANYONGE NA WASIOJIWEZA

Njia hii ni nzuri sana katika kujikinga mtu na shari zote zikiwemo pamoja na shari za mahasidi wachawi na wenye vijicho. Mtenda mema ni mpenzi wa Allaah. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Fanyeni wema (ihsani); hakika Allaah huwapenda wafanyao wema (wenye ihsani)."** [al-Baqarah: 195]. Kutokana na mapenzi hayo, Allaah hawezi kukubali hata kidogo kumuona mpenzi wake anadhurika na shari ya mchawi, hasidi na mwenye kijicho bila ya kumpa nusura dhidi ya shari hizo. Aidha mtenda mema hupata shukrani nyingi kutoka kwa anaowatendea wema, shukrani ambazo hugeuka kuwa ni duwa kubwa kwake ya kuzidishwa mema yake na kueposhiwa kila baya litakaloelekezwa dhidi yake.

KUOMBA HIFADHA NA KINGA KWA ALLAAH KUTOKANA NA SHARI ZA WACHAWI, MAHASIDI NA WENYE VIJICHO: Qur'aan inatufundisha hivyo katika Suratul Falaq. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Sema; ninajikinga kwa Mola wa Ulimwengu wote. Na shari ya alivyoviumba. Na shari ya Giza la usiku liingiapo. Na shari ya wale wanaopuliza (vuvia) mafundoni, wakavunja mashikamano yaliyo baina ya watu, yaani shari ya mafatani, na shari ya hasidi anapohusudu."** [al-Falaq: 1-5]. Allaah ni msikivu wa maombi ya mwenye kutaka hifadha kwake, na ni mjuzi mno wa shari za maadui wake, aidha Allaah ameahidi kujibu maombi ya mwenye kumuomba. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na Mola wenu anasema: Niombeni Nitakujibuni."** [Gaafir: 60].

Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametufundisha Adkaar (nyiradi) nyingi za kuzitumia wakati wa kumuomba Allaah hifadha na kinga ya wachawi, mahasidi na wenye vijicho. Kumvumilia mchawi, hasidi na mwenye kijicho ni dawa kubwa sana, na ni njia mojawapo ya kuwafanya maadui hao wajione kuwa ni wajinga wao wenyewe, aidha subira ya mtu humletea faida nyingi "Subira huvuta kheri, na Allaah siku zote yuko pamoja na wenye kusubiri. Miongoni mwa kheri za subira, ni kupata usaidizi wa Allaah wa kumnusuru na maadui wake. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Ndio namna hivi. Na alipizaye kisasi sawa na dhara aliyotiwa, kisha akadhulumiwa tena, Allaah atamsaidia. Hakika Allaah ni mwingi wa msamaha (na) Mwingi wa Maghfira."** [Al-Hajj: 60]. Ikiwa katika aya hii tunafahamishwa yakuwa Allaah anamsaidia mwenye kulipiza ovu alilotendewa; itakuwaje basi kwa yule ambaye hakulipiza baada ya kutendewa ovu! Bilashaka huyu atapata msaada zaidi.

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

KUMPUUZA ADUI NA KUTOMPATILIZA VITENDO WALA KIMAWAZO: Hii pia ni njia nyengine mojawapo ya kujiokoa mtu na shari za wachawi, mahasidi na wenye vijicho. Na hii inatokana na kuwa katika elimu ya nafsi tunaambiwa: 'Mtu anapolihofia jambo na kulitia moyoni, basi hata kama jambo hilo ni la kawaida kwake litakuwa ni la kimiujiza. Na anapolidharau jambo na kutolitilia maanani, basi hata kama jambo hilo ni la hatari kiasi gani yeye kwake litakuwa kama chawa wa kubanjwa na vidole viwili tu.'

KUZIMA MOTO WA HASIDI, MCHAWI NA MWENYE KIJICHO KWA KUWATENDEA WEMA: Pamoja na kuwa njia hii ni nzito sana (ki-binadamu) lakini ni njia mwafaka kabisa katika kuwashinda waovu hao. Nasema ni nzito kwa sababu vipi mtu akufanyie ubaya wa waziwazi kabisa kisha wewe ulipize ubaya huo kwa kumtendea wema! Bila shaka yataka moyo na imani ya hali ya juu na subira kubwa. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"mambo mazuri na mabaya hayawi sawa. Ondosha (ubaya unaofanyiwa kwa wema); tahamaki yule ambaye baina yako na baina yake kuna uadui atakuwa kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia uchungu. Lakini (jambo hili) hawatapewa ila wale wanaosubiri, wala hawatapewa ila wenye hadhi kubwa (kwa Allaah).**" [Fusswilat: 34-35].

Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametuhadithia kisa cha mmoja wa Mitume wa Allaah iliyotangulia, yakwamba siku moja alipigwa na jamaa zake mpaka akatolewa damu, wakati damu hiyo inamtoka Mtume huyo alisema: "*Ewe Mola wangu, wasamehe jamaa zangu, hakika wao ni watu wasiojua.*" Angalia hakusema, "*Ewe Mola wangu, waangamize makafiri hawa, kwa sababu ni mijitu mijinga isiyojua kitu.*" Lakini alisema kwa sauti ya huruma, "*Ewe Mola wangu:*

* Wasamehe (anawatakia msamaha
* Jamaa zangu (amejinasibisha na wao na kujikurubisha kwao)
* Hakika wao nio watu wasiojua (anawatolea udhuru kwa makosa yao

Jee ndugu msomaji, waonaje maneno kama haya ya upendo ukiyatoa kwa adui yako; ataendeleza kweli uadui wake kwako au atasimamisha? Bila shaka maneno haya ya kunyong'onyeza viungo hata mtu awe ni adui kiasi gani nina uhakika wa asilimia mia moja (100%) yakuwa ataacha na uadui wake badala yake atakuwa mtu mwema kwako na rafiki mzuri sana.

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) "*Zimeumbwa* nyoyo za watu kumpenda anayewatendea wema na kumchukia anayewatendea mabaya."

HITIMISHO: Hizi ndizo sababu kumi za kujikinga na shari zote za Mahasidi, wachawi na wenye vijicho. Na hakuna jambo muhimun katika yote kama kumuelekea Allaah, na kumtegemea Yeye peke yake wakati wa matatizo. Na mtu anatakiwa aelewe yakuwa atakapoelekeza tumaini lake kwa asiyekuwa Allaah, basi Allaah humnyima hifadha na kinga yake na humuachia huyo anaemtegemea asiyekuwa Yeye (Allaah). Huu ndio utaratibu wa Allaah, na hakuna awezae kuubadilisha utaratibu huu. Sasa ndugu yangu msomaji, utakapokuwa wewe umenyimwa hifadha ya Allaah, Bwana wa viumbe wote unatarajia kupata hifadha ya nani?

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 4)

4. Katika kubadilika kwa matamshi ya ahaadeeth zinazohusiana na Najd, inakuwa hapana shaka kulihusu lizungumzwalo.

a)Hadeeth ya Ibn 'Umar iliyopokelewa na Abu Nu'aym katika al-Hilya (6/133), *"Ewe Allaah Tubariki katika Madeenah yetu, na Utubariki katika Makkah yetu, na Utubariki katika Shaam yetu, na Utubariki katika Yemen yetu, na Utubariki katika vipimo vyetu (fee saa'inaa wa muddinaa)."* Akasema mtu mmoja, "Ewe Mtume wa Allaah, na katika Iraaq yetu." basi akageuka kuangalia kando na akasema, *"(huko) kutatokea zilzala (mitetemeko), fitna, na maafa na kutatokeza pembe ya Shaytaan."* Shu'ayb al-Arna'ut akaipasisha isnaad yake kuwa ni saheeh kama ilivyo katika maelezo yake ya 'Sharh as-Sunnah' (14/206-207 fn.2), nae pia akaridhia maneno ya al-Khattaabee tuliyo yadondoa hapo awali.
b) Hadeeth ya Ibn 'Umar iliyopokelewa na at-Tabaraanee katika kitabu cha 'Al -Awsat' yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliswali swala ya Alfajiri kisha akawaelekea watu na akasema, *"Ewe Allaah Tubariki katika Madeenah yetu, Ewe Allaah Tubariki katika vipimo vyetu, Ewe Allaah Tubariki katika Shaam yetu na Yemen yetu."* Akasema mtu mmoja, "Na Iraaq Ewe Mtume wa Allaah?" Akasema, *"kutoka hapo itachomoza pembe ya Shaytaan na fitna na maafa yatatokea kama milima ya mawimbi."* Ibn Hajar al-Haythamee akasema katika kitabu chake cha 'Mujma az-Zawaaid' (3/305 - mlango 'Ukusanyaji wa Du'a zilizo ombewa (Madeenah)'): 'Wapokezi wake ni waaminifu na ni watu wa kisawasawa.' [Hadeeth hii huwenda ikafikiriwa kuwa sawa na ile ya b) hapo juu, lakini nimeiweka kando kwa ajili ya tafauti ndogo katika maneno, Allaah yanamuelea zaidi.] c) Hadeeth ya Ibn Abbaas iliyopokelewa na at-Tabaraanee katika kitabu chake cha 'al-Kabeer' yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliomba Du'a na akasema, *"Ewe Allaah Tubariki katika Shaam yetu na Yemen yetu."* Mtu mmoja miongoni mwa watu waliokuwepo akasema, "Na Iraaq Ewe Mtume wa Allaah?" Akasema, *"Kwa hakika hapo iko Pembe ya Shaytaan, na fitna na maafa yatatokea kama milima ya mawimbi, na kwa hakika udhalimu/ukatili uko mashariki."* AL-Haythamee akasema: 'Wapokezi wake ni waaminifu na ni watu wa kisawasawa.

Utukufu wa Bani Tameem. Wengi katika kizazi cha Bani Tameem ni wakaazi wa Najd iliyoko Saudi Arabia.
a) Katika hadeeth iliyopokelewa na Abu Hurairah (Radhiallaahu 'anhu) kutoka katika saheeh al-Bukhaaree: "Niliwapenda watu wa kabila la Bani Tameem tangu nilipomsikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiwataja (Bani Tameem)

ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO

Amesema Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم); *"Ewe Allaah Tubariki katika Shaam yetu; Ewe Allaah Tubariki katika Yemen yetu."* Wakasema watu, "Ewe Mtume wa Allaah, na Najd yetu." Nafikiri mara ya tatu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema, *"Hapo (Najd) patatokea zilzala (mitetemeko), fitna na maafa, na pembe ya Shaytaan itatokeza kutoka huko."* [Imepokewa na Bukhaaree (katika mlango wa 'Fitna itatokeza kutoka Mashariki' 9/166 no. 214 tafsiri ya Ki-Ingereza).

Hadeeth iliyoviringwa na mabishano kutokamana na sababu za vikundi fulani. Hadeeth ambayo iliyopotolewa (kwa makusudi) na vipote fulani vya watu ili wapate kueneza upotofu wao wapate kuwashawishi Waislamu wajinga.

Jambo hili, kwa kutokana na utafiti, uchunguzi na upekuzi wa maneno ya Wanavyuoni wa kale, tutaona yakwamba hadeeth hii haihusiani na Najd iliyo mashuhuri iliyoko Saudi leo, lakini inahusiana na Iraaq.

Kiasi cha miaka miwili nilisoma kitabu kilichoandikwa hususan kuhusu hadeeth hii kinachoitwa, "an-Najd Qarnu ash-Shaytaan" [nimemsahau muandishi na kwa vile kitabu hicho mimi sinacho tena] Nitajaribu kuwa muangalifu katika kuyadondoa kwa ujumla nitakayo yakumbuka kutoka katika kitabu hicho, na nitajiepusha kuzinukuu sehemu halisi za kitabu hicho isipokuwa zile kumbukumbu nilizozifanyia utafiti mimi mwenyewe. Miongoni mwa Wanavyuoni walioihusisha hadeeth hii na Iraaq ni: al-Khattaabee, al-Kirmaanee, al-Aynee, an-Nawawee, Ibn Hajar na wengineo. Sababu za msimamo wao ni nyingi na ziko wazi-wazi.

Umaarufu wa hadeeth kuhusu fitna zinazokuja kutoka sehemu za Mashariki.

AL-Bukhaaree akaiweka hadeeth hii kwenye mlango: "Fitna itajitokeza katika sehemu za Mashariki"

212) Imepokewa Kutoka kwa Babake Saalim: Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisimama kando ya mimbar (na akaashiria kuelekea mashariki) na akasema: *"Fitna iko huko! Fitna iko huko! ambako pembe ya Shaytaan inapojitokeza"* au alisema, *"pembe ya Jua"*

213) Imepokewa kutoka kwa Ibn 'Umar aliyesema: Nimemsikia Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) akisema haliyakuwa ameelekea sehemu za mashariki: *"Kwa hakika fitna iko huko, kutokako pembe ya Shaytaan."*

214) Hadeeth za Najd zinaendelea kujadiliwa.

1. Hadeeth mithili ya hizo zinapatikana katika Saheeh Muslim (vol.4 no.6938+). Na ahaadeeth zenye kumaanisha mfano wake zinapatikana katika Saheeh Muslim (Vol.1 no.83+).

2. Kwa ujumla, fitna na maafa yaliyotokea katika wakati wa mwanzoni yalichipuka kutoka katika sehemu za mashariki, na kwa hakika yalitokea ndani ya Iraq kwenyewe. Baada ya kuyadondoa maneno ya al-Khattaabee katika kuifafanua maana ya Qarn (pembe), Ibn Hajar al-Asqalaanee akasema: "na kuna wale wasemao yakwamba watu wa mashariki walikuwa ni makafiri katika wakati ule na Mtume (صلى الله عليه وسلم), akatueleza yakwamba fitna na maafa yatajitokeza kutoka sehemu hiyo na yakatokea kama alivyosema. Na fitna za mwanzo kutokea, zilijitokeza kutoka katika sehemu hizo za mashariki na ndio zikawa sababu za kutengana kwa Waislamu, na hayo ndiyo ayapendayo na kuyasherehekea Shaytaan. Vile vile mambo ya uzushi yalijitokeza kutoka katika sehemu hizo." [Fath al-Baaree 13/58 katika kusherehesha hadeeth ya Najd] Miongoni mwa fitna zilizowahi kuzuka katika nchi ya Iraaq na sehemu za mashariki ni mauaji ya 'Alee, mauaji ya mjukuu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم), vita miongoni mwa Waislamu wenyewe kwa wenyewe na mengine mengi. Imaam an-Nawawee akataja miongoni mwa fitna kubwa zitakazotokea kutoka katika sehemu za mashariki itakuwa ni kutokea kwa Dajjaal. [Sharh Saheeh Muslim 2/29] Miongoni mwa mambo ya uzushi yaliyowahi kutokea kwenye sehemu za mashariki hususan Iraaq, ni idadi ya vipote vya upotofu katika zama za awali, wakiwemo Qadariyyah (kama inavyo-onyesha kwenye hadeeth ya kwanza katika saheeh Muslim), wakiwemo Jahmiyyah na vizazi vyao... Katika wakati wa Mtume (صلى الله عليه وسلم), inategemea pale mtu alipo, lakini kulikuwa na mahali 13 pakijulikana kwa jina la Najd [kulingana na 'Najd Qarnu ash-Shaytaan']. Sababu ni kwamba, neno Najd, ki-lugha lina maana ya kilicho inuka, ardhi iliyo nyanyuka. Kwahivyo, ardhi ambazo zilizoinuka, Waarabu walikuwa wakizipa jina la Najd. Mojawapo ya ardhi mashuhuri za Najd katika wakati huo zilikuwa ni Iraaq. Najd kwa wale watu waliokuwa wakiishi Madeenah wakielekea upande wa mashariki itakuwa ni Iraaq. Akasema Ibn Hajar: "Amesema al-Khattaabee: 'Najd iliyo upande wa mashariki, na kwa yule aliye katika Mji wa Madeenah, basi Najd yake itakuwa ni jangwa la Iraaq na pambizoni mwake [baadiya al-Iraaq wa Nawaaheehaa], kwani sehemu hii ni mashariki ya watu wa Madeenah. Maana ya kimsingi ya Najd ni sehemu iliyoinuliwa/ardhi iliyo nyanyuliwa kutoka ardhini iliyo kinyume cha al-Gawr, ambayo ni sehemu iliyo chini. Tihaamah [mwambao wa pwani ya kusini-magharibi na ufuo wa kusini mwa Bara-Arabu] yote hiyo ni al-Gawr na mji wa Makkah umo ndani ya Tihaamah."

3. Ibn Hajar akaendelea, "Kutokana na maneno haya (ya al-Khattaabee), udhaifu wa maneno ya ad-Dawoodee yamefahamika yakwamba 'Najd iko katika upande wa Iraaq' [min Naahiyah al-Iraaq] kwani rai yake ni kwamba Najd ni mahali maalum. Hali haikuwa hiyo, bali kila kilichoinuka ukilinganisha na kilichopakana nacho ni Najd na hiyo sehemu ya chini ni Gawr." [Fath al-Baaree 13/58-59] Al-Haafidh al-Mubaarakfooree akayaunga mkono maneno haya katika sherhe yake ya Sunan at-Tirmidhee (10/314 no. 4212)

4. Hadeeth iliyo katika Saheeh Muslim [4/1505 no.6943] Amesema Saalim bin 'Abdullaah bin 'Umar yakwamba: "Enyi watu wa Iraaq, mbona mnashangaza nyinyi mambo yenu, mwauliza kuhusu madhambi madogo kisha mwafanya madhambi makubwa? [mauaji ya al-Husayn] Nilimsikia babangu, 'Abdullaah bin 'Umar akisimulia yakuwa alimsikia Mtume wa Mwenyzi Mungu (صلى الله عليه وسلم) akisema na huku akiashiria kuelekea sehemu za mashariki kwa mkono wake: *"Kwa hakika fitna itajitokeza kutoka upande huu utakaotokeza pembe ya Shaytaan na mutachinjana wenyewe kwa wenyewe..."*

(Endelea Katika Ukurasa wa 3)